

## 1. الجُفْ Al-Jawf - Uwazi wa kinywa na koo<sup>1</sup>

Katika sehemu hii ya uwazi wa kinywa na koo kunapatikana makhraj moja tu ambamo hutoka herufi tatu za madd; nazo ni:

Alif	ا	Iliyo na sukuwn na kabla yake kuna fat-hah inatamkwa 'aa'
Waw	و	Iliyo na sukuwn na kabla yake kuna dhwammah inatamkwa 'uw'
Yaa	ي	Iliyo na sukuwn na kabla yake kuna kasrah inatamkwa 'iy'

Wakati wowote ule herufi hizi tatu zikiwa hazifungamani na sharti hizo zilizotajwa basi huwa na matokeo mengine kwani wakati huo huwa si herufi za madd. Na herufi tatu hizi zimekusanyika katika kauli ya Allaah: **نُوحِيَهَا (nuwhiyaha)**

## 2. الْخُلْقُ Al-Halq - Koo<sup>2</sup>

Katika al-Halq (koo) kuna makhaarj tatu ya herufi sita.

i- أَقْصَى الْخُلْقِ Aqswal-halq - Mbali ya koo (mwishoni karibu na kifua)

Zinapotoka herufi za ه و ئ

---

<sup>1</sup>Herufi hizi juu ya kuitwa kuwa ni herufi za Jawfi; pia hueleweka kama ni herufi za maddiyah (za madd) na herufi za hawaaiyyah (herufi za hewa)

<sup>2</sup>Herufi hizi huitwa na kueleweka kama ni herufi za halqiyyah au herufi za idhwhaar.

ii- وَسْطُ الْخُلْقِ Waswatwul-halq - Katikati ya koo

Zinapotoka herufi za ح ع

iii- أَدْنَى الْخُلْقِ Adnal-halq - Koo la karibu (na mdomo)

Zinapotoka herufi za خ غ